**Maurice Cuthbert, (b. 1919)**

Maurice Cuthbert alikuwa mtoto wa mmishonari mtangulizi katika Afrika Mashariki, aliyeitwa William Cuthbert. Maurice alikuwa mmisionari na msimamizi wa kanisa katika Afrika Mashariki, Kati, na Kusini mwa Afrika.

**Maisha ya Awali**

Maurice Cuthbert alizaliwa huko Southampton, Uingereza, takribani mwaka wa 1919. Wazazi wake William na Florence Cuthbert walihudumu kama wamishionari katika Konferensi ya Uingereza Kusini iliyokuwa na makao yake huko Southampton. William Cuthbert aliwahi kuwa katibu wa idara aliyesimamia misheni zilizo kwenye fildi. Mnamo 1922, baba yake alikubali mwito wa kuwa mmisionari nchini Kenya na kuhamia Gendia pamoja na familia yake, ambayo ilijumuisha wana wawili, Raymond na Maurice. Maurice Cuthbert alikuwa mtoto tu wakati huo. Baadaye alihamia Tanganyika na wazazi wake wakati baba yake alipowekwa kuwa msimamizi wa vituo mbalimbali vya misheni Kanda ya Ziwa. Cuthbert alijifunza kuzungumza Kiswahili na akaijua vizuri lugha hiyo. Baba yake alipojiuzulu kutoka kwenye huduma ya kichungaji mnamo 1931, familia ilihamia Eldoret ambapo baba yake alichukua ardhi huko Lemook na kuwa mkulima. Shamba lao lilipakana na Hifadhi ya Nandi na wengi wa wafanya kazi wao wa shambani walikuwa Wanandi. Akiwa hapa aliishi maisha ya mtoto mlowezi.

**Somo la Maisha kwa Maurice**

Wakati mmoja, mwaka wa 1937, mama yake Cuthbert, aitwaye Florence, alikabiliana waziwazi na msimamizi wa shamba lao, Kili araap Randich, ambaye alikuwa amemuagizia amletee mayai. Ilibainika baadaye kuwa baadhi ya mayai aliyomletea yalikuwa mabaya. Kili alisihi kuwa hana hatia akisema kuwa hajui kuhusu kuwepo kwa mayai hayo mabaya kwani alikuwa ametumwa tu na mkewe kupeleka mayai hayo. Florence Cuthbert alikasirika sana na kumrudishia Kili mayai yote huku akimrushia moja ya yai lililooza. Hili lilikuwa tusi kubwa kwa mwanaume Mnandi ambaye alijivunia sana uanaume wake.

Kili araap Randich (“mwana wa Randich”) ambaye alikuwa mrefu, mwenye umbo kubwa alijizuia na kubaki mtulivu utulivu mbele ya tukio hilo alilolitafsiri kama tusi kubwa, akageuka kimya kimya na kuondoka zake. Kijana Cuthbert, wakati huo akiwa katika ujana wake, alishuhudia mtafaruku huo kimya kimya. Kisha akamfuata Kili huku akimzonga kwa maneno mengi ya kuudhi, jambo ambalo watoto wengi wa kikoloni walikuwa wamezoea kulifanya. Cuthbert alikuwa ameathirika na mazoea ya watoto walowezi ambao walijulikana kwa ukorofi na majivuno, hasa kwa wafanyakazi wao Waafrika. Hata hivyo, safari hii, Kili alipoteza utulivu wake na kwa fimbo aliyokuwa ameshika, alimpiga Cuthbert kichwani kwa nguvu huku akiacha shimo la kina. Akaondoka zake kwa utulivu huku yule kijana aliyemwaga damu akiomboleza kwa maumivu makali. Mama yake alimsaidia, akiapa kumfanya Kili alipe kitendo chake.

Alimkimbiza Cuthbert katika hospitali ya Eldoret. Baada ya kushonwa, alitumia siku kadhaa kupata nafuu hospitalini.

Kili araap Randich aliacha kazi yake na kuondoka shambani, na kurudi kwenye nyumba yake mahali alipohisi ni salama zaidi ndani kabisa ya Hifadhi ya Nandi. Kipigo hicho kilimtia kiwewe sana kijana Cuthbert na, labda kwa kuona makosa ya ujana wake, na kupitia uzoefu ule tabia yake ilibadilika. Alibadilishwa na kumkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wake. Alibatizwa katika Kanisa la Waadventista mnamo Septemba 1938 baada ya kampeni ya uinjilisti iliyoandaliwa na kuendeshwa na wainjilisti, akiwemo na baba yake mwenyewe.

Mnamo 1939, alijiunga na King's African Rifles kutumika katika jeshi wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. Akiwa jeshini aliwahi kuliandikia gazeti la The Advent Survey akiwashukuru kwa kumpelekea nakala za gazeti hilo, Signs of the Times, ambalo yeye na maofisa wenzake walifurahia.

**Msiba Shambani, Kuhamia Afrika Kusini**

Msiba uliikumba familia hiyo aliporudi baada ya vita mwaka wa 1945. Mnamo Juni, babake aliuawa shambani baada ya mapigano mabaya na mmoja wa wafanyakazi wake. Mfanyakazi huyo alishindwa kufuata maagizo fulani na William Cuthbert alimkabili kimwili. Mfanyakazi, Chepsiror araap Butuk, akiwa ameshika panga, alimchoma vibaya Cuthbert. Butuk, alipoona alichokifanya, alikimbia kutoka shambani na kujiua. Baada ya kifo cha mumewe, Florence Cuthbert aliuza shamba na kuondoka na wanawe kwenda Afrika Kusini. Maurice Cuthbert alijiandikisha katika Chuo cha Helderberg kusomea uchungaji. Alifuata nyayo za baba yake, akawa mmishonari. Baada ya mafunzo yake, alirudi Kenya na kujihusisha kikamilifu na kanisa, akipanda hadi kuwa katibu na mweka hazina wa South Kenya Field (sasa Conference) kupitia sehemu kubwa ya miaka ya 1950.

**Kufanya kazi kama Mmishonari**

Mwaka 1955, aliondoka Kenya na kuelekea Tanganyika ambako aliendelea kuwa Katibu-Mhazini wa Misheni ya Tanganyika yenye makao yake makuu Busegwe maili ishirini kutoka Musoma kaskazini mwa Tanganyika. Kama ilivyotajwa hapo awali, baba yake alikuwa mhudumu mwenye bidii miongoni mwa Wanandi, akiwaleta kwenye imani ya Waadventista Wanandi kadhaa ambao waliingia ndani kabisa ya Hifadhi ya Nandi wakieneza Uadventista. Mmoja wa wale waliokuja kuwa Waadventista kutoka kazi ya Cuthbert alikuwa Philip araap Kili, mtoto wa mshambuliaji wa Maurice Kili araap Randich. Kabla ya kuja kufanya kazi kama msimamizi katika shamba la Cuthbert, Kili araap Randich alikuwa msimamizi wa shamba la Ndege la David Sparrow. Ingawa hakuwa Muadventista, mwanawe alijiunga na kanisa.

Mnamo Septemba 1958, Philip Kili alihudhuria Kongamano la Vijana la Afrika Mashariki lililofanyika Nairobi. Philip alikuwa kiongozi wa vijana wa mtaa na alikuja na ujumbe mkubwa wa vijana kutoka Nandi. Kongamano hilo lililoleta wajumbe kutoka Union ya Afrika Mashariki nzima, lilihudhuriwa na Maurice Cuthbert, mjumbe kutoka Tanganyika. Hapa Philip alikutana na Cuthbert ambaye sasa alikuwa mtu mzima na kumtambua mara moja. Baada ya kujitambulisha na kumkumbusha Cuthbert tukio la shambani kwao, Cuthbert alipatwa na hisia kali sana na walikumbatiana kwa mahaba na kuhitimisha maisha yao ya nyuma. Cuthbert alifurahi kukutana na mtoto wa mvamizi wake na Philip akagusa kovu la tukio hilo la bahati mbaya.

Walishangaa kwamba Mungu alikuwa amewaleta pamoja katika familia ya Waadventista licha ya asili zao tofauti kabisa. Kwa njia fulani, baba yake Kili alikuwa "amemwongoza" Maurice Cuthbert kwa Kristo kwa sababu huko ndiko alikoamua kuchukua matembezi ya karibu zaidi pamoja na Yesu. Philip na Cuthbert wakawa marafiki wa karibu kuanzia hapo.

**Kazi Zaidi ya Umishonari**

Maurice Cuthbert alibaki Busegwe hadi muda mfupi baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1962 alipoondoka kuelekea Afrika Kusini. Aliendelea na ajira ya kanisa na akapata kazi katika Jumba la Uchapishaji la Sentinel huko Kenilworth, Cape Town, ambako alihudumu kama meneja mauzo. Alitawazwa kwa kuwekewa mikono ya uchungaji mwaka wa 1963 na kuhamia Johannesburg ambako aliendelea kufanya kazi katika Kanisa akifanya hasa kazi za utawala. Alikua mkaguzi wa hesabu za Union ya Afrika Kusini mnamo 1966 na alihudumu hadi 1969 alipohamia Rhodesia (sasa Zimbabwe) ambapo alihudumu kama katibu wa elimu katika fildi ya Mashonaland. Mkewe pia alikua mmishonari aliyeidhinishwa katika fildi ya Mashonaland. Wakati huo, akina Cuthbert walikuwa wafanyakazi pekee wasio Waafrika katika fildi mzima.

Mnamo 1971, Cuthbert alihamia tena kaskazini hadi fildi ya Zambia ambako alifanya kazi kama Katibu-Mhazini huko Chisekesi, Zambia. Hii ilikuwa mara yake ya kwanza kufanya kazi katika taifa huru la Afrika. Pia alijiunga na bodi ya Hospitali ya Mwami na Leprosarium nchini Zambia. Mnamo 1979, akina Cuthbert walirudi Afrika Kusini na kuishi Transvaal, wakiendelea kufanya kazi kwa Kanisa. Cuthbert aliwahi kuwa mkaguzi wa hesabu za Union ya Kusini. Alistaafu mwaka 1984 na kuhamia Uingereza ambako aliishi siku zake zote. Binti yake Denise pia alihamia Uingereza ambako alifanya kazi kwa huduma ya Usimamizi wa Hatari ya Waadventista (Adventist Risk Management Services) huko St. Albans.